

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA BUTIAMA**

Shule ya Sekondari Kukirango,

S.L.P 871,
MUSOMA

Tarehe:

Namba za simu:

Mkuu wa shule – 0767 960 690

Makamu Mkuu wa Shule – 0756 798 315

MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI.....

SHULE YA MSINGI

S.L.P

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KUKIRANGO KIDATO CHA
KWANZA MWAKA 2021**

1.0. UTANGULIZI

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya Sekondari Kukirango mwaka 2021. Hongerasana.

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe **11/01/2021**. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **11/01/2021** kwa ajili ya kujisajili na tayari kuanza Masomo.

2.0 MAHITAJI MUHIMU YA SHULE

2.1. Sare ya shule (Uniform).

(a) Kwa Wavulana:

- i) Suluali nyeusi mbili (2) zenye marinda mawili na mifuko mitatu; miwili pembeni na mmoja nyuma. Suruali isiwe modo na upana wa suruali usipungue inchi 16.
- ii) Mkanda mweusi wa ngozi wenye bakoli ya kawaida.
- iii) Hauruhusiwi kufunga ndevu na kunyooa mitindo ya kihuni.

(b) Kwa Wasichana:

- i) Sketi nyeusi mbili (2) zisizobana, na ziwe ndefu zinazogusa kiatu zenye michirizi nyeupe miwili katikati mbele ya kila sketi.
- ii) Hauruhusiwi kusuka nywele.

(c) Kwa Wasichana na Wavulana:

- i) Shati nyeupe mbili (2) zenye mikono mifupi na zisizo na urembo wowote na Tai nyeusi urefu usivuke mkanda wa suruali au sketi.
- ii) Soksi nyeupe fupi jozi mbili (2) zisiwe na urembo wowote.
- iii) Viatu vya ngozi nyeusi vya kufunga na kamba, vyenye visigino vifupi na visivyopiga kelele wakati wa kutembea kwenye sakafu., vyenye kufunika miguu na visivyo na urembo wowote, wala kuchongoka mbele.
- iv) Sweta rangi ya **“Dark blue”** mikono mirefu.
- v) “T- Shirt” rangi nyekundu yenye shingo ya duara ikiwa na nembo ya shule hii.

vi) Picha mbili (2) kwa ajili ya kuweka kwenye “file” lenye taarifa binafsi za mwanafunzi.

NB: Kumbuka kushona kitambaa kizito cha suti na siyo kitambaa cha sukari sukari kwa ajili ya suluali au sketi.

(d) Utaratibu wa uvaaji wa Hijab kwa Waislam

- i) Hijab mbili (2) Rangi nyeupe kitambaa kisiwe chepesi.
- ii) Blauzi iwe (nusu kanzu) pana ya mikono mirefu isiyofunika viganja vya mikono
- iii) Blauzi iwe ndefu inayoshuka chini ya makalio (isiwe kama gauni)
- iv) Kitambaa cha kichwani (ushungi) kiwe kipana kirefu kisichofunika viganja vya mikono wala uso.

(e) Sare ya Michezo:

Kwawavulanani – Bukta nyeusi na Raba.

Kwawasichanani – Sketi nyekundu na Raba.

2.2 VIFAA VYA KUTUMIA DARASANI NA WAKATI WA MITIHANI

- i) Madaftari makubwa yasiyopungua 12 (Counter Book Quire 2).
- ii) Rimu moja (1) ‘Double A’(kwa ajili ya Mazoezi, Majaribio na Mitihani atakayokuwa akifanya hapa shuleni).
- iii) Mkebe wa Hisabati (Mathematical set) na “Mathematical table”(Four figure).
- iv) Kalamu za “blue” au nyeusi za kutosha muhula.
- v) Rula ndefu 1 na Penseli za kutosha muhula.
- vi) Kamusi ya Kiingereza kwa Kiingereza (Oxford English Dictionary– English/English).
- vii) Faili moja ya plastiki kwa ajili ya kutunza kumbakumbu za mwanafunzi.

3.0 CHAKULA

Kwa shule za kutwa. Chakula ni jukumu la Mzazi au Mlezi ivo utapewa utaratibu na shule wa namna ya kufanikisha zoezi hili.

4.0 MATIBABU

Shule haitowi huduma ya matibabu kwa wanafunzi hivyo gharama za tiba zitakuwa chini ya mzazi / mlezi wa mwanafunzi mwenyewe. Shule itatoa huduma ya kwanza tu kwa matatizo madogo.

5:0 SHERIA, KANUNI NA TARATIBU MUHIMU ZA SHULE HII:

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebisha na sheria namba 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya elimu nchini. Hivyo ni muhimu kwako kumkumbusha mwanao ajue umuhimu wa sheria za shule. Ni ukweli usiopingika kwamba malezi ya wanafunzi kitaaluma kiroho na kimwili yanategemea ushirikiano kati ya walimu na wazazi.

Mwanafunzi anatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na atapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

- i) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- ii) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.
- iii) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
- iv) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- v) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
- vi) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
- vii) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

ADHABU:

Mwanafunzi atakaye kiuka utaratibu huu atasimamishwa masomo (suspension) na endapo atarudia atafukuzwa shule kabisa.

5.1 MAKOSA YAFUATAYO YANAWWEZA KUSABABISHA UKAFUKUZWA SHULE MARA MOJA.

1. Wizi
2. Uasherati
3. Ubakaji
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kamab vile uvutaji Bangi, Cocaine, Milungi, Kubeli n.k
5. Kupigana na kupiga
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma
7. Kudharau bendera ya Taifa
8. Kuoja au kuolewa
9. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
10. Kugoma, kuchochea au kuongoza au kuvunja amani na usalama wa shule au watu.
11. Kukataa adhabu kwa makusudi.
12. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi shuleni.

6.0. MAMBO MENGINE MUHIMU

Mzazi utatakiwa kukamilisha na kuleta viambatisho au fomu zifuatazo:

(a) Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form)

Mwanafunzi apimwe katika Hospitali ya Serikali na Mganga anayehusika kukamilisha vipengele vya afya yake . Fomu hii itakabidhiwa ofisini kwa Mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.

(b) Fomu ya maelezo binafsi

Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya Mwanafunzi / mkataba wa kutoshiriki katika Migomo, Fujo na Makosa ya jinai na;

(c) Kiapo cha Mzazi / Mlezi kukiri kukubaliana na sheria

Fomu ya Mzazi / Mlezi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

7.0 MWISHO

Mwanafunzi anatakiwa kusoma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu. Zaidi ya hapo, mwanafunzi anapaswa kutumia akili au ufahamu wa kawaida, yaani “COMMON SENSE” katika kufanya maamuzi.

TANIBIHI:

Mazazi / Mlezi wa mwanafunzi aliyechaguliwa kujiunga na shule hii unaombwa kumleta mwanao juma la kwanza la masomo linaloanza tarehe 11/01/2021 bila kukosa.

J.M BALWETEGILE
MKUU WA SHULE YA SEKONDARI KUKIRANGO.

**HALMASHAURI YA WILAYA YA BUTIAMA
FOMU HII UIJAZWE MAPEMA NA KUIKABIDHI SIKU YA KWANZA UNAPOPOKELEWA
SHULENI**

SEHEMU A:

Tarehe ya kuripoti shuleni

Jina langu halali ni Kabila

Tarehe ya kuzaliwa Mwezi Mwaka

Tarehe ya kuchanjwa Ugonjwa ni

Jina la Baba au Mlezi Kazi ya Baba/Mlezi

Namba ya simu Anwani

Taja majina ya ndugu wa karibu walioko karibu na shule watakaoruhusiwa kumtembelea mtoto wako akiwa hapa shuleni (ijazwe na mzazi / mlezi)

Na.	Jina la ndugu	Uhusiano	Anakoishi	Namba ya simu
1.				
2.				
3.				

SEHEMU B: TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI

Jina la mwanafunzi

Wazazi wako wote wapo Hai? Ndiyo / Hapana

Kama jibu ni Hapana taja mzazi yupi yupo Hai Baba / Mama / Wote hawapo Hai (kata isiyohusika)

Unalelewa na nani kwa sasa?

.....

.....

Mimi

Nakiri kwamba natambua na kutumia nafasi niliyoipata ya kuendelea na elimu ya Sekondari. Nafahamu kwamba Mzazi / Mlezi wangu anasaidia gharama ya elimu hii na sehemu kubwa inagharamiwa na Umma wa Tanzania. Kwa sababu hii naahidi kuitumia nafasi hii niliyoipata kupata mafanikio yanayolenga kulikwamua Taifa letu changa.

Naahidi kuwa na nidhamu, Utii na kufuata maelekezo ya WALIMU na viongozi, na nitakubali makosa na kufanya adhabu husika bila kusita au ubishi.

MUNGU wangu naomba unisaidie kutimiza wajibu kama Mwanafunzi kwa kipindi cha miaka minne niwapo hapa shuleni.

Jina Sahihi Tarehe

Jina na sahihi ya Mzazi / Mlezi

Jina na Sahihi ya Afisa Mtendaji wa Kijij / Mtaa

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

**Kukirango Secondary School,
P.O.Box 871,
MUSOMA.**

Date:

PART A:

TO THE MEDICAL OFFICER,

.....
.....
.....

RE: **(Full name of student)**

Please kindly examine the above, named as to his/her Physical and mental fitness enrolment as a secondary school student. The examination should include the following categories.

1. (a) Eye-sight (b) Hearing (c) Limbs (d) Speech
 (e) Venereal diseases (f) Leprosy (g) Epilepsy
2. Neurosis
3. Pregnancy
4. Other serious diseases

PARTB

MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by a Government Medical Officer)

I have examined the above named person and consider that he/she is physically FIT / UNFIT and Mentally FIT / UNFIT or full time of schooling.

1. (a) Eye-sight.....
- (b) Hearing.....
- (c) Limbs.....
- (d) Speech.....
- (e) Venereal diseases.....
- (f) Leprosy.....
- (g) Epilepsy.....
2. Neurosis.....
3. Pregnancy.....
4. Other serious diseases.....

Date:.....

Signature of Examiner:.....

Station:.....

Designation:.....

KIAPPO CHA KUTII KANUNI/ SHERIA ZA SHULE NA TAARIFA MUHIMU ZA MWANAFUNZI.

SEHEMU YA AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi

Ninakiri na kuahidi kuwa nitatii sheria na kanuni za shule. Iwapo nitakiuka, hatua za kinidhamu zichukuliwe dhidi yangu kwa kadri inavyostahili. Pia naahidi kuwa nitawajibika vema katika Masomo Darasani na Kazi zote nitakazopangiwa Shuleni kwa utii wa hali ya juu na Mungu anisaidie.

Sahihi ya Mwanafunzi

Tarehe

SEHEMU YA AHADI YA MZAZI / MLEZI WA MWANAFUNZI

Mimi

Ambaye ni Mzazi / Mlezi wa(Jina la Mwanafunzi)

nakiri na kuahidi kuwa nitatoa ushirikiano mzuri kwa Uongozi wa Shule katika kumlea Kijana wangu. Hii ikiwa ni pamoja na kumtimizia mahitaji yote ya shule kwa wakati. Nitakuwa tayari kushirikiana na Uongozi wa shule katika suala zima la nidhamu ya Mwanafunzi na kwamba pale itakapolazimu kuitwa shuleni, kwa suala la Utovu wa nidhamu wa Mwanafunzi, nitakuwa tayari kuitika wito.

Sahihi ya Mzazi/Mlezi

Tarehe

**J.M BALWETEGILE
MKUU WA SHULE YA SEKONDARI KUKIRANGO.**